**UWATA PRE & PRIMARY ENGLISH MEDIUM SCHOOL**

S.L.P 3574,
MBEYA.

Mobile: +255-754-3522-278
+255- 763-278-870
+ 255- 754-960-938

**Email:info@uwataprimary.ac.tz**
**MOTTO: "EDUCATION IS OUR LIBERATION"**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA SHULE YA MSINGI UWATA - 2024**

**MZAZI/MLEZI WA: ……………………………………………………………**
**FOMU NAMBA:……………………..….**

***Uongozi wa shule ya awali na msingi UWATA, unapenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule ya UWATA. Unakaribishwa sana. Fomu hii ina maelezo yote muhimu hivyo unaombwa kuisoma kwa umakini mkubwa.***

## SEHEMU A: MAELEKEZO YA AWALI:

1. Shule ipo katika eneo la Sae karibu na kituo cha nguvu za umeme wa TANESCO Mbeya mjini kandokando ya barabara ya DAR – MBEYA.
2. Shule hii ni ya bweni na kutwa na inachukua wanafunzi wavulana na wasichana wa dini zote.
3. Shule itafunguliwa tarehe 8/01/2024.

## B. SARE ZA SHULE ( UNIFORM )

Mzazi /Mlezi ufuatao ni uvaaji wa nguo za shule siku za masomo:

| *SIKU* | *AINA YA SARE YA SHULE* |
|---|---|
| JUMATATU | SARE YA SHULE ( KAWAIDA) |
| JUMANNE | SARE YA SHULE ( KAWAIDA) |
| JUMATANO | TRUCKSUTI YA SHULE , T-SHETI NA RABA NYEUSI |
| ALHAMISI | SARE YA SHULE ( KAWAIDA) |
| IJUMAA | TRAKSUTI YA SHULE , T-SHETI NA RABA NYEUSI |

Mzazi/Mlezi zingatia kwamba **sare ya shule zinapatikana shuleni na si vinginevyo**. Sare zitakazoshonwa nje ya shule hazitakubalika. **Zitakuwa na lebo maalum ya shule**.

### GHARAMA ZA NGUO ZA SHULE

i. **Gharama za uniform kwa mwanafunzi wa kutwa ni sh. 141,000/=**
( mwanafunzi atapewa shati 2, suruali/sketi 2, T- shirt 1, neck tie 1, tracksuit 1, sweta 2, mzura 1)

ii. **Gharama za uniform kwa mwanafunzi wa bwenini sh. 241,000/=**
( mwanafunzi atapewa shati 2, suruali/sketi 2, t- shirt 1, neck tie 1, tracksuit 1, sweta 2, mzura 1, nguo za bweni jozi 2, trucksuit ya bweni 1 na mashuka 2).

**Malipo ya nguo za shule (Uniform) yalipwe kwenye akaunti ya michango CRDB 0150654080000 JINA: UWATA EDU - CENTRE MICHANGO.**

**MAHITAJI YA BWENI.**

**Vifaa vya Bweni vya kutokanavyo nyumbani :-**

a) Sabuni katon 2 za miche
b) Sabuni ya unga kilo 2.
c) Sabuni za kuogea 10
d) Godoro 6 kwa $2\frac{1}{2}$
e) Jozi mbili za viatu vyeusi kwa wavulana
f) Mikanda miwili rangi nyeusi kwa wavulana
g) Jozi moja ya viatu vya michezo ( Raba nyeusi )
h) Pull neck 2 (nyeusi na nyeupe)
i) Jacket nyeusi
j) Blanketi moja
k) Track suit ya rangi nyekundu
l) Bukta moja na vesti 6 ( kwa wavulana)
m) Khanga jozi moja kwa wasichana vesti 5
n) Kiwi kopo kubwa moja brushi na kishungi
o) Nguo za ndani 5 au zaidi kwa wasichana na wavulana
p) Mafuta ya kupakaa ya mgando kopo kubwa 2 na glycerine 1
q) Kitana na sabuni za kuogea 6
r) Dawaza meno 2 kubwa na miswaki 5
s) Ndoo ndogo ya kuogea
t) Yebo 1 ngumu na taulo 1
u) Tight ( taiti ) 4 kwa wasichana
v) Soksi zisipungue jozi 5.

***Mzazi /Mlezi kumbuka kuandika majina kamili matatu katika vitu vyote vya mwanao ili kuepuka upotevu, uandikie nyumbani.***

## SEHEMU C: ADA NA MICHANGO MINGINE

**1. ADA**

Mchanganuo wa ulipaji wa ada na mihula ya shule kwa mwaka 2024

| ***S/N*** | ***DARASA*** | ***AINA YA HUDUMA*** | ***KIASI*** | ***JANUARI*** | ***APRIL*** | ***JULY*** | ***SEPTEMBER*** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | TZS | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 | VII | BWENI | 1,992,000 | 996,000 | 498,000 | 498,000 | |
| | | | | | | | |
| 2 | I,II,III,IV,V &VI | WANAO KAA BWENI | 1,940,000 | 485,000 | 485,000 | 485,000 | 485,000 |
| | | | | | | | |
| 3 | I,II,III,IV, & V | WANAOTUMIA USAFIRI | 1,712,000 | 428,000 | 428,000 | 428,000 | 428,000 |
| | | | | | | | |
| 4 | I,II,III,IV, & V | WASIOTUMIA USAFIRI | 1,372,000 | 343,000 | 343,000 | 343,000 | 343,000 |

**Muhimu:** Ada ilipwe kwa wakati ili kuepuka usumbufu, malipo ya ada yafanyike kupitia akaunti zifuatazo:-

I. **CRDB – 01J1065414700** Jina la account: **UWATA EDUCATION CENTRE.**
II. **NMB – 61302300186** Jina la account: **UWATA EDUCATION CENTRE.**

Kumbuka kuandika majina kamili matatu ya mwanafunzi na darasa, baada ya hapo leta mwenyewe bank slip hiyo shuleni (ofisi ya uhasibu).

**ZINGATIA:** *Mwanafunzi yeyote ambaye hatafikisha kiwango cha ada kilichoainishwa kwa awamu husika hatapokelewa kabisa. Mzazi tunaomba ushirikiano wako katika hili.*

2. **MICHANGO MINGINE**

Mwanafunzi atatakiwa kulipia **mchango wa masomo ya ziada (remedial classes na uchakavu (maintenance) sh. 100,000/=**pesa hii inalipwa kwa awamu mbili kwa mwaka Januari sh **50,000/=** na julai **sh 50,000**/= na kama utaweza kulipa yote januari ni sawa . Lipa kwenye akaunti ya michango **CRDB 0150654080000 JINA: UWATA EDU-CENTRE MICHANGO.**

## SEHEMU D: MAAGIZO YA TAALUMA.

I. Mwanafunzi anatakiwa kuleta **rimu 2** (Januari rimu moja na Julai rimu moja)
II. Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi wa darasa la I - VII hakikisha unamnunulia vifaa vya kitaaluma vifuatavyo:-

| S/N | DARASA LA I - II | DARASA LA III - IV | DARASA LA V - VII |
|---|---|---|---|
| 1 | Daftari ndogo 10 za mistari mikubwa na midogo na 2 ziwe za vyumba ( Daftari) za kurasa 200 jaladia kwa jalada la kaki). Daftari hizo zipokelewe na mwalimu wa darasa la I – II siku ya kufungua shule. | Madaftari madogo 15 ya kurasa 200. | Madaftari makubwa (counter book) 1 za quire 3 (counter book) 6 za quire 2 na daftari ndogo 7 zenye kurasa 200 na zijaladiwe na jalada la kaki. |
| 2 | Penseli 25 za HB halisi. | Vitabu vya ziada kulingana na masomo. | Vitabu vya ziada kulingana na masomo. |
| 3 | Vifutio 2 na vichongeo 2. | Pen 12, penseli 5 rula 1 na vifutio 5. | Mkebe na vifaa vya uchoraji |
| 4 | Penseli za rangi (crayons) . | Counter book 1 kwa ajili ya somo la hisabati. | Atlas 1 (for primary school). |

## SEHEMU E: SHERIA ZA SHULE

Mzazi unataarifiwa kuwa msingi mkuu wa shule ya UWATA ni NIDHAMU na TAALUMA. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia na kuheshimu sheria zote za shule. Kinyume cha hapo adhabu stahiki zitachukuliwa dhidi yake. Sheria zifuatazo zitasimamiwa kulinda Nidhamu ya shule kwa manufaa ya mwanafunzi na taifa kwa ujumla.

1. Mwanafunzi anatakiwa kutumia lugha nzuri (asitumie lugha chafu) anapowasiliana na wenzake au na mtu yeyote
2. Mwanafunzi haruhusiwi kuondoka shuleni bila ruhusa maalumu
3. Mwanafunzi anatakiwa kuwa safi mwili na sare zake za shule, kuvaa nguo chafu na zilizochanika ni kinyume na sheria za shule

4. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wasio walimu na watu wote kwa ujumla
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shuleni asubuhi kabla ya saa moja na nusu, na anatakiwa kuhudhuria mstarini bila kukosa.
6. Mwanafunzi anapaswa kufanya mawasiliano yote kwa kutumia lugha ya kiingreza awapo shuleni muda wote
7. Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza mazingira ya shule
8. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zake na za wenzake
9. Ni mwiko kwa mwanafunzi kupigana
10. Hairuhusiwi kuvuta sigara, kunywa pombe au kutumia madawa ya kulenya
11. Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki kusikiliza neno la Mungu
12. Ni marufuku mwanafunzi kuzini, au kufanya vitu vyovyote vinavyoashiria uzinzi
13. Ni marufuku mwanafunzi kuiba mali za wengine au za shule
14. Ni mwiko mwanafunzi yeyote kuruka ukuta/ fensi
15. Ni marufuku mwanafunzi kusuka, kujichubua au kujipamba kwa heleni n.k

ASANTE SANA KWA KUIAMINI SHULE YA MSINGI UWATA KARIBU SANA SHULENI UWATA NA MUNGU AKUBARIKI SANA.

**MUNGU AWABARIKI.**

HEAD MISTRESS
UWATA PRE & PRIMARY ENGLISH MEDIUM SCHOOL
P. O. BOX 3574 MBEYA

______________________

**BERTILA D. MFAUME**

**(MKUU WA SHULE)**